Uzoefu wa Wokovu

“Kwa upendo usio na kifani na rehema, Mungu alimfanya Kristo asiyejua dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, kusudi katika Yeye tuweze kufanywa haki ya Mungu. Tukiongozwa na Roho Mtakatifu, tunatambua hitaji letu, na kukiri hali yetu ya dhambi, tunatubia uasi wetu, na kuonyesha imani katika Yesu kama Bwana na Kristo, kuwa mbadala na Kielelezo chetu. Imani hii inayopokea wokovu huja kupitia uwezo wa kimbingu kwa Neno nan i karama ya neema ya Mungu. Kupitia Kristo tunahesabiwa haki, kufanywa wana na binti wa Mungu, na kuokolewa kutoka katika mamlaka ya dhambi. Kupitia Roho Mtakatifu tunazaliwa upya na kutakaswa; Roho hufanya upya nia zetu, huandika sheria ya Mungu ndani ya mioyo yetu, na tunapewa uwezo wa kuishi maisha matakatifu. Tukikaa ndani Yake tunakuwa washirika wa hali ya asili ya uungu na kuwa na hakika ya wokovu sasa na katika siku ya hukumu. (2Kor.5:17-21; Yoh.3:16; Gal.1:4; 4:4-7; Tit.3:3-7; Yoh. 16:8; Gal.3:13, 14; 1Pet.2:21, 22; Rum.10:17; Luk.17:5; Mk. 9:23, 24; Efe.2:5-10; Rum.3:21-26; Kol.1:13, 14; Rum.8:14-17; Gal.3:26; Yoh.3:3-8; 1Pet.1:23; Rum.12:2; Ebr.8:7-12; Eze.36:25-27; 2Pet.1:3, 4; Rum.8:1-4; 5:6-10).”

Maisha ya Mkristo ambaye Roho wa Mungu anakaa ndani yake (Rum. 8:9) hayawezi yakabaki yaleyale. Kristo alilipenda Kanisa hata akajitoa kwa ajili yake ili alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno apatae kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa (Efe. 5:25-27). Utakaso wa jinsi hiyo ndilo lengo la Kanisa. Washiriki wa Kanisa wanaweza wakakiri kwamba “ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya kila siku (2 Kor. 4:16). Kwa hiyo tunaakisi utukufu wa Bwana, tukibadilishwa tufanane nao, toka utukufu hadi utukufu (2 Kor. 3:18).

Kwenye maandiko, uzoefu wa muumini wa wokovu yaani kuhesabiwa haki, kutakaswa, kusafishwa, na kukombolewa kunaelezewa kuwa (1) kumekamilika (2) kunaendelea kukamilishwa (3) kutakamilishwa wakati ujao. Kuelewa mitazamo hii kutaondosha misuguano inayotokana na kutokuelewa.

Uzoefu wa Wokovu na Wakati Uliopita

Kujua kuhusu Mungu na pendo lake hakutoshi. Jitihada isiyomhusisha Yesu kamwe haitaleta matunda ya wokovu. Yesu alisema, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu (Yoh. 3:3). Wokovu hupatikana kwa Yesu peke yake (Mdo. 4:12). Yesu ndiye njia na kweli na uzima (Yoh. 14:6). Uzoefu wa wokovu hujumuisha kutubu, kuungama, msamaha, kuhesabiwa haki na kutakaswa.

1. Kutubu (toba). Roho alipogusa mioyo watu waliokuja kuhiji siku ya Pentekoste, Petro aliawaambia tubuni (Mdo. 2:37, 38 Mdo. 319).

Maana ya kutubu*:* Neno kutubu / toba, hutokana na neno la Kiebrania *nachum* lenye maana ya kuhuzunika, kusikitika. Neno la Kigiriki lenye maana sawa na hilo ni *metanoeo,* lenye maaana ya kubadilisha mawazo/nia. Utambuzi wa afichaye dhambi zake hatafanikiwa (Mith. 28:13), huongoza mtu kuungama maovu yake maalum. Toba hufikia kilele kwa kuongoka (Mdo. 15:3).

Mfano wa toba inayoongoza kwenye ushindi wa dhambi ni toba ya Daudi. Aliomba asamehewe na kuumbiwa moyo mpya (Zab. 51:3, 1, 10). Uzoefu wa baadaye wa Daudi unadhihirisha kwamba msamaha wa Mungu siyo kwamba husamehe dhambi, bali pia huokoa kutoka dhambini.

Japokuwa toba inatangulia msamaha, mwenye dhambi hawezi kujipatia baraka ya Mungu yeye mwenyewe. Toba ni karama inayotolewa na Mungu (Mdo. 5:31 Rum. 2:4)

Msukumo wa kutubu: Yesu alikufa tulipokuwa tungali wenye dhambi (Rum. 5;6-10). Hakuna kinachogusa moyo kama upendo wa Yesu unaosamehe (Yoh. 12:32). Huo ndio wema unaotuvuta kutubu (Rum. 2:4).

2. Kuhesabiwa Haki. Kwa upendo na rehema visivyo kifani, Mungu alimfanya mwana wake dhambi ili sisi tuwe haki ya Mungu (2 Kor.5:21). Kwa njia ya imani, moyo hujazwa na Roho Mtakatifu. Na kwa imani hiyo hiyo ambayo ni kipaji kutoka kwa Mungu cha neema (Rum. 12:3 Efe. 2: 8), mwenye dhambi atubuye huhesabiwa haki (Rum. 3:28).

Neno kuhesabiwa haki hutumika kuwasilisha kitendo cha Mungu cha kumtangaza mwenye dhambi kuwa ana haki. Ni kinyume cha kuhukumiwa (Rum. 5:16). Kuhesabiwa haki siyo kwa sababu ya matendo yetu. Ni kwa sababu mtu mmoja alitii, nasi tunahesabiwa haki (Rum. 5:18, 19). Utii wa Yesu unafanywa kuwa utii wa mdhambi bure (Rum. 3:24), siyo kwa sababu ya utii wetu bali kwa neema yake (Tito 3:5).

Kuhesabiwa haki na matendo. Wengi wetu huamini uwongo kwamba kusimama kwetu mbele za Mungu kunategemea matendo yetu yawe mema au mabaya. Paulo alifundisha kwa msisitizo wokovu uliotolewa bure na Mungu. Tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa kwa imani iliyo katika Kristo (Wafil. 3:8, 9). Ibrahimu alihesabiwa haki kwa imani (Rum. 4:3, Mwa. 15:6). Alihesabiwa haki kabla ya kutahiriwa na siyo kwa sababu ya kutahiriwa (Rum. 4:9,10). Ni imani gani Ibrahimu alikuwa nayo?

Kwa imani Ibrahimu alipoitwa, alitii “aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa kuwa urithi…” (Ebr. 11:8-10, Mwa. 12:4, Mwa. 13:18). Kwamba alikuwa na imani ya kweli, kulidhihirishwa na matendo yake. Mtume Yakobo alionya juu ya uwongo mwingine wa imani isiyo na matendo. Kwa Ibrahimu, imani yake ilidhihirishwa na matendo kwa kumtoa Isaka (Yak. 2:21). Hivyo imani hukamilishwa na matendo (Yak. 2:22). Kama imani haina matendo imekufa (Yak. 2:17). Hivyo imani inayohesabiwa haki ni imani iliyo hai, yenye kufuatiwa na matendo (Yak. 2:24).

Uzoefu wa Kuhesabiwa Haki. Tunapohesabiwa haki, Yesu ambaye hakuijua dhambi alifanywa dhambi ili sisi tupate haki yake ya kuwa wana wa Mungu (1Kor. 5:21). Kama wadhambi wenye kutubu, tunapokea kwa kipimo tele, msamaha mkamilifu. Mungu husema kama ilivyokuwa kwa Joshua, hiki si kinga kilichotoka motoni? (Zek. 3:2). Ndipo hutamka “tazama nimekuondolea uovu wako, nami nitakuvika mavazi ya thamani nyingi (Zek. 3:4). Dhambi zilizoungamwa huwekwa kwa Yesu na Mdhambi aliyetubu hupokea haki ya Yesu.

Matokeo ya Kuhesabiwa Haki

1. ***Kutakaswa.*** Neno kutakaswa humaanisha kufanywa mtakatifu.Toba ya kweli na kuhesabiwa haki huongoza kwenye kutakaswa. Utakaso nayo ni kazi ya neema ya Mungu. Hatua tatu za kutakaswa zinazofundishwa na Biblia ni (1) ni jambo lililokwisha kutimizwa (2) ni jambo linaloendelea kutimizwa sasa katika maisha ya mkristo (3) ni jambo litakalokamilishwa Yesu akirudi. Kwa wakati uliopita, wakati mtu anapohesabiwa haki, pia huwa amepokea utakaso kwa jina la Bwana Yesu (1Kor. 6:11 cf. Yoh. 15:3). Kama matokeo ya kuitwa na Mungu (Rum. 1:7) waumini huitwa watakatifu kwa kuwa wako katika Kristo (Wafil. 1:1, Yoh. 15:1-7).

2. ***Kufanywa watoto wa Mungu.*** Wakati huo huo tunapokea Roho ya kufanywa wana na warithi pamoja na Yesu (Rum. 8:15-17). Ni fursa bora kiasi gani, raha iliyoje?

3. ***Kuthibitishiwa wokovu.*** Kuhesabiwa haki kunatuthibitishia kuwa ukombozi wetu ni hakika (Efe. 1:7)

4. ***Mwanzo wa maisha mapya ya ushindi.*** Kutambua kwamba dhambi zetu zilizopita zimefunikwa, huleta uponyaji katika maisha yetu. Imani yetu kwake ikiongezeka, uponyaji wetu na kubalishwa nako kutaongezeka. Kuushinda kwake ulimwengu hutupatia garantii kwa wokovu wetu juu ya dhambi (Yoh. 16:33)

5. ***Zawadi ya Uzima wa Milele.*** Mahusiano yetu mapya na Yesu hutupatia zawadi ya uzima wa milele. Aliye na mwana ana uzima wa milele, asiye na mwana hana uzima (1Yoh. 5:12)

Uzoefu wa Wokovu na Wakati wa Sasa
Kwa damu ya Yesu kutupatia kuhesabiwa haki, kutakaswa, kusafishwa, muumini anakuwa kiumbe kipya na ya kale hupita (2Kor. 5:17)

Wito wa kuishi maisha matakatifu. Wokovu hujumuisha kuishi maisha matakatifu kwa msingi wa kile Yesu alichotufanyia msalabani. Paulo alitoa wito kwa waumini kuishi maisha ya maadili (1Thes. 4:7). Ili waweze kuishi maisha matakatifu, Mungu huwezesha kwa kutoa Roho (Rum. 1:4), kwa kadiri ya utajiri wa neema yake (Efe. 3:16, 17). Kwa kuwa ni viumbe vipya, waumini wanayo majukumu mapya (Rum. 6:12-14, 19). Sasa wataishi kwa kuongezwa na Roho (Gal. 5:25).

Waumini waliojawa na Roho hawatembei kwa jinsi ya mwili bali kwa roho. (Rum. 8:1 cf 8:4). Wanabadilishwa kwamba kuishi kimwili ni mauti (Rum. 8:6) na kwa kuwa wana Roho, basi hawako kimwili bali kiroho (Rum. 8:9). Lengo lao kuu ni kumtukuza Mungu (1Thes. 4:1), wakiepuka zinaa na kudhulumu ndugu (1Thes. 4:3, 6, 7).

Mabadiliko ya Ndani
Siku Yesu atakapokuja mara ya pili tutabadilishwa mwili wa kufa uvae kutokufa, wenye kuharibika, uvae kutokuharibika (1Kor. 15;51-54). Hata hivyo, mabadiliko ya tabia yanapaswa kuendelea kwa ajili ya kumlaki Yesu ajapo mara ya pili. Mabadiliko ya ndani huhusisha utu wa ndani na hufanyika kila siku (2 Kor. 4:16, Rum. 12:2).

1. ***Kumhusisha Yesu na Roho Mtakatifu.*** Ni mwumbaji tu ndiye awezaye kukamilisha kazi ya uumbaji kutubadilisha maisha yetu (1Thes. 5:23). Hata hivyo hatafanya hivyo pasipo kutushirikisha. Ni Roho ndiye atendaye kazi ya kumfunua Kristo na kurejesha ndani yetu taswira ya Mungu iliyopotea (Rum. 8:1-10).

Mungu hutamani kukaa ndani yetu kwa kuwa ameahidi hivyo (2Kor. 6:16, cf. Yoh. 3:24, 4:12). Paulo alisema Kristo huishi ndani yangu (Gal. 2:20, cf. Yoh. 14:23). Kuishi ndani yetu kwa Mungu hutubadilisha kila siku (2Kor. 4:16) na kutubadilisha nia zetu (Rum. 12:2, Wafil. 2:5).

2. ***Kushiriki asili ya Uungu.*** Ahadi kubwa mno ya Yesu ni kutupatia uwezo kukamilisha mabadiliko ndani yetu (2Pet. 1:4). Kuufikia uwezo wa kimbingu hutusaidia kutoka imani hadi wema, maarifa, kiasi, saburi, utauwa, upendano wa ndugu hadi upendo (2Pet. 1:5-7). Kuwa na karama hizo hutuepusha na uvivu na kukosa matunda, kwani akosaye hayo ni kipofu (2Pet. 1:8, 9)

a) Kupitia Kristo Pekee. Kinachobadilisha wanadamu hadi kufikia kushiriki asili ya uungu ni kumvaa Kristo (Rum. 13:14, Ebr. 3:14) na kufanyanywa upya na Roho Mtakatifu (Tit. 3:5). Ni kukamilisha upendo wa Mungu ndani yetu (1Yoh. 4:12).

b) Ni mchakato unaoendelea. Kutakaswa ni zoezi la kuendelea. Kwa maombi na kujifunza Maandiko (kumla Yesu) Matakatifu tunaendelea kushirikiana na Mungu. (Yoh. 6;53-56). Maneno nisemayo ni roho na ndiyo uzima (Yoh. 6:63, pia Mt. 4:4)

1. ***Mabadiliko ya kiaina***
   (a) Mungu anatumaini kuwabadili wanadamu walioanguka nia, mawazo, matamanio na tabia hata wajae matunda ya Roho (Efe. 5:27, Gal. 5: 22,23)
   (b) Mungu hutulinda tusianguke (Yud. 24). Maisha ya kiroho ni ya mabadiliko ya daima. Hakuna nafasi ya katikati linapokuja ufalme wa Mungu na wa Shetani (Rum. 6:17, 18). Yule atawalaye mawazo yetu, ndiye atutawalaye sisi. Ikiwa tunamchagua Kristo atutawale fikra (2Kor. 10:5) yeye ndiye anayekuwa mtawala wetu.

Ukamilifu wa Kristo
Ukamilifu wa Biblia ni nini, unapatikanaje?

Ukamilifu wa Biblia
Neno la kiebrania linalowakilisha ukamilifu ni *tam* au *tamim* lenye maana ya kutimia, vema, kamili, isiyo na doa. Kwa kigiriki, neno *teleios* humaanisha kukamilika, kukomaa. Kwenye Agano la Kale limetumika kuelezea maana iliyopungua. Nuhu, Ibrahimu na Ayubu wanaelezewa kuwa walikuwa wakamilifu (Mwa. 6:9; 17:1, 22:18 Ayu. 1:1, 8) lakini nao walikuwa na mapungufu yao (Mwa. 9:20, 21 na Ayu. 40:2-5) Katika Agano Jipya, ukamilifu huelezea mkristo aliyeishi kwa uaminifu kadiri ya nuru aliyonayo (cf. 1Kor.14:20; Wafil. 3:15; Ebr. 5:14). Tumeitwa kuwa wakamilifu (Mt. 5:48) na kwa neema ya Mungu twaweza kushangilia ushindi (cf. Kol. 4:12, Yak. 3:2).

1. ***Ukamilifu katika Kristo.*** Roho Mtakatifu hutuletea ukamilifu wa Kristo. Kwa imani, ukamilifu wa Kristo unakuwa wetu. Bila Kristo haiwezekani (Yoh. 15:5). Kristo ndiye hekima ya Mungu, utakatifu na ukombozi (1Kor. 1:30). Tunatimilika utimilifu wa Mungu (Efe. 3:19)

2. ***Kukaza mwendo kufikia ukamilifu.*** Kupitia Kristo akaaye ndani yetu twaweza kufikia utimilifu wa Kristo (Efe.4:13), na kuondokana na uchanga wa imani (Efe. 4;14), na kuweza kula chakula kigumu yaani kupambanua mema na mabaya (Ebr.5:14). Kwa nafasi yetu ya kuwa Wakristo, tunaitwa kukaza mwendo kufikia utimilifu (Ebr. 6:1) uliojaa matunda (Wafil.
1:9-
11).

Maisha matakatifu siyo maisha yasiyo ya matatizo. Tumeitwa kutimiza wokovu kwa kuogopa na kutetemeka (Wafil. 2:12, 13). Tuonyane…kushikamana na mwanzo wa uthabiti kwa nguvu hadi mwisho (Ebr. 3:13, 14, cf. Mt. 24:13). Maandiko huonya, tukitenda dhambi kusudi, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi (Ebr. 10:26). Hivyo, maombi yasiyokoma ni muhimu kwa maisha ya utakaso na ukamilifu (Kol. 1:9, 10)

Kuhesabiwa haki kila siku

Kuna wakati hatuwezi kuyatambua makosa yetu (Zab.19:12) kwa kuwa moyo hudanganya (Yer. 17:9). Kwa hali hiyo, tunaambiwa tusitende dhambi, ila kama mtu ametenda dhambi, tunaye mwombezi kwa Baba (1Yoh. 2:1). Tukiungama, tunasamehewa (1Yoh. 1:9)

Uzoefu wa Wokovu na Wakati Ujao

Wokovu wetu hatimaye hukamilika tunapokuwa tumefufuliwa na kuvikwa kutokufa au kunyakuliwa mbinguni. Hilo ndilo tumaini la utukufu wa Mungu (Rum. 5:2). Ujio wa Yesu mara ya pili pia unaleta wokovu (Ebr. 9:28).

Kuvikwa Utukufu na Kutakaswa. Kuwa na Yesu moyoni ni sharti la kuokoleaw siku za usoni kwa kuvikwa utukufu (Kol. 1:27). Kwa Roho anayekaa ndani yetu, miili yetu itahuishwa (Rum.8:11). Ni jambo la kushukuru kwamba tangu mwanzo tulichaguliwa kupata wokovu, tunatakaswa na tutavikwa utukufu (2Thes. 2:13, 14). Katika Kristo, tayari tuko kwenye kiti cha enzi cha Mungu mbinguni (Kol. 3:1-4). Tayari tumeonja enzi ijayo (Ebr. 6:4, 5). Tukimwangalia Yesu na kutafakari utukufu wake, tunabadilishwa kutoka utukufu hadi utukufu (2Kor. 3:18). Sasa hivi tunaugua tukisubiri ukombozi wa miili yetu (Rum. 8:19, 23 cf. Efe. 4:30). Kuvikwa utukufu kutafanyika katika wakati uliowekwa na Mungu (Mdo. 3:21) wakati ulimwengu utakapofanywa upya (Mt. 19:28) kutimiza ukombozi hata wa viumbe vingine (Rum. 8:21)

Kuvikwa Utukufu na Kukamilishwa. Wako wanaoamini kwa uwongo kwamba ukamilifu utakaoletwa na utukufu wa Mungu tayari upo kwa wanadamu. Paulo alikataa jambo hilo kabla ya kufa kwake, aliposema siyo kwamba nimekwisha kufika, nakaza mwendo, niifikile mede ya dhahabu (Wafil. 3:12-14). Aliyesimama na aangalie asianguke (1Kor. 10:12). Historia ya Daudi, Sulemani na Petro ipo kutufundisha juu ya hayo.

Msingi wa Kukubaliwa kwetu na Mungu. Siyo kule kuwa na tabia ya Yesu au kutokuwa na doa kunakomfanya Mungu atukubali.Haki inayookoa inatoka kwa mwenye haki mmoja, Yesu Kristo na huwasilishwa kwetu na Roho Mtakatifu. Hakuna aliye na haki isipokuwa Kristo (Rum. 3:10), mwanadamu alivyo ni mavazi yaliyotiwa unajisi (Isa. 64:6, pia Dan. 9:7, 9, 11, 20 na 1Kor. 1:30). Kristo ndiye haki yetu nasi tunatakaswa ndani yake. (1Kor. 1:30).